Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania
MKURABITA

DESEMBA 2020

YALIYOMO

YALIYOMO……..…i
ORODHA YA MAJEDWALI……iv
VIFUPISHO VYA MANENO…….v
KAULI YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UONGOZI……..vi
NENO KUTOKA KWA MRATIBU WA MPANGO……...vii
KAMATI YA UONGOZI WA MKURABITA……..…viii

SURA YA KWANZA……..1
UTANGULIZI……..1
1.1 MKURABITA Kwa Muhtasari……1
1.2 Lengo la Kuanzishwa MKURABITA……..……1
1.3 Mantiki……..…2
1.4 Mchango wa MKURABITA katika Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa…….2
1.4.1 MKURABITA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025…...……2
1.4.2 MKURABITA na Ilani ya CCM, 2015……...…..3
1.4.3 MKURABITA na FYDP II……..……4
1.5 Awamu za Utekelezaji……...……4
1.6 Dira na Dhima ya MKURABITA……..……5
1.7 Tunu za Msingi……..……..6
1.8 Wadau wa MKURABITA……6
1.9 Mfumo wa utekelezaji/Uendeshaji…….…..……7
1.10 Mpangilio wa Taarifa…….…….……7

SURA YA PILI……..…8
UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA URASIMISHAJI RASILIMALI ARDHI…….……..8
2.1 Uandaaji na utoaji wa Hati Miliki…….8
2.1.1 Uandaaji na Utoaji wa Hati Miliki za Kimila Tanzania Bara…8
2.1.2 Urasimishaji wa Ardhi Mjini……..14
2.1.3 Uandaaji na Utoaji wa Hati za Haki za Matumizi ya ardhi Zanzibar…….14
2.2 Ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji……...16

SEHEMU YA TATU……..17
UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA URASIMISHAJI BIASHARA…….……17
3.1 Kujenga Uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara……..…17
3.1.1 Kutoa Mafunzo kwa Wadau wa Urasimishaji……..18
3.1.2 Kutoa fedha kwa ajili ya uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara……..19
3.1.3 Kutoa Vifaa katika Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara……..19
3.2 Uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara……20
3.3 Mafunzo ya urasimishaji kwa wamiliki wa Biashara……..…..21
3.4 Usajili wa biashara……22
3.5 Utafiti wa Msingi……23

SURA YA NNE…….……28
KUJENGEA UWEZO WAMILIKI WA ARDHI NA BIASHARA……..…28
4.1 Mafunzo ya kutumia Hati Miliki kupata Mikopo……..…..30
4.2 Ushiriki wa wanawake kwenye mafunzo……31
4.3 Mafunzo ya Uendelezaji Biashara…….……...31

SURA YA TANO…….……33
UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA HUDUMA SAIDIZI……..……..33
5.1 Habari na Mawasiliano……..…..33
5.2 Uratibu wa Mapendekezo ya Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi ……35
5.3 Ufuatiliaji na Tathmini……36
5.3.1 Ufuatiliaji na Tathmini…… Error! Bookmark not defined.
5.3.2 Ziara za Viongozi za Kukagua Utekelezaji……37

SURA YA SITA ……...41
MATOKEO YA URASIMISHAJI…… . 41
6.1 Matokeo ya urasimishaji kwa wananchi..... 41
6.1.1. Wanufaika kujumuishwa kwenye huduma za fedha..... 41
6.1.2. Ongezeko la Utunzaji wa kumbukumbu..... 41
6.1.3. Upatikanaji wa Mikopo ya wamiliki wa biashara..... 42

6.1.4. Upatikanaji wa mikopo kwa Wamiliki wa ardhi…… 43
6.1.5. Upatikanaji wa Ajira…… 44
6.1.6. Kuongezeka kwa Usalama wa miliki…….. 45
6.2 Matokeo ya Urasimishaji kwa Taifa…….. 46
6.2.1. Ongezeko la Mapato yatokanayo na leseni za biashara.. 46
6.2.2. Uendelevu wa shughuli za urasimishaji…… 47
6.2.3. Kupungua kwa migogoro ya ardhi…….. 47

SURA YA SABA…… 48
RASILIMALI WATU NA FEDHA…… 48
7.1 Rasilimali watu…… 48
7.2 Mafunzo kwa watumishi……48
7.3 Vyanzo vya Fedha na Utekelezaji wa Bajeti…… 49
7.5 Ukaguzi wa Fedha za Utekelezaji……49

KIAMBATISHO Na. 1:
REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE PROPERTYAND BUSINESS FORMALIZATION PROGRAM FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020……49

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: MKURABITA katika Kufikia Malengo ya NDV 2025 3
Jedwali Na. 2: Hali ya Uhakiki wa Mashamba 2019/2020..... 9
Jedwali Na. 3: Taarifa ya Uhakiki na Uandaaji wa Hati Miliki za Kimila 11
Jedwali Na. 4: Hali ya Umiliki wa mashamba kwa jinsi..... 13
Jedwali Na. 5: Hali, uandaaji na utoaji wa hati za Viwanja Zanzibar, 2019/20 15
Jedwali Na. 6: Wadau walioshiriki Mafunzo ya Urasimishaji .**Error! Bookmark not defined.**
Jedwali Na. 7: Utoaji wa Vifaa vya urasimishaji Biashara Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/20 19
Jedwali Na. 8: Wamiliki wa biashara waliopata mafunzo Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/2020..... 22
Jedwali Na. 9: Usajili wa Biashara Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/2020 23
Jedwali Na. 10: Hali ya Vyanzo vya Mitaji kwa asilimia 27
Jedwali Na. 11: Idadi ya Wakulima na Viongozi waliopata mafunzo ya kujenga uwezo 2018/2020..... 31
Jedwali Na. 12: Muhtasari wa Matokeo ya Tathmini ya Uendelevu na Faida za Urasimshaji Ardhi Itigi na Mufindi, 2019/2020 **Error! Bookmark not defined.**
Jedwali Na. 13: Bajeti, Fedha iliyopokelewa na Matumizi kwa mwaka 2019/2020 49

VIFUPISHO VYA MANENO

BRELA	Business Registration and Licensing Agency (*Wakala ya Usajili wa Leseni na Biashara*)
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CCROs	Certificate of Customary Right of Occupancy (*Hati za Haki Miliki za Kimila)*
COVID 19	Corona Virus Disease 19 *(Ugonnjwa unaosababishwa na virusi vya korona vya mwaka 2019)*
FYDP I	Five Years Development Plan I *(Mpango wa Kwanza waMaendeleo wa Miaka Mitano)*
FYDP II	Five Years Development Plan II *(Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano)*
MKURABITA	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania
MKUKUTA II	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania Awamu ya Pili
MSM	Mamlaka za Serikali za Mitaa
NDV 2025	National Development Vision 2025 *(Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025)*
NSSF	National Social Security Fund (*Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii*)
SIDO	Small Industries Development Organization (*Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo*)
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (*Chama cha Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania*)
TIN	Tax Payer's Identification Number (*Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi*)
TRA	Tanzania Revenue Authority (*Mamlaka ya Mapato Tanzania*)

KAULI YA MWENYEKITI WA KAMATI YA UONGOZI

Kwa niaba ya Kamati ya Uongozi ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Mwaka 2019/2020 ya MKURABITA kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2020. Taarifa ya Mwaka 2019/2020 ya MKURABITA ni ya kwanza kutolewa na imeeleza shughuli zilizofanywa kwa mwaka 2019/2020 na mafanikio yaliyopatikana. Kupitia taarifa hii, inaonekana dhahiri kwamba urasimishaji wa rasilimali na biashara za wananchi ni nyenzo ya kupunguza umaskini wa kipato kwa mwananchi mmoja mmoja na hatimae kukuza uchumi wa taifa letu. Matokeo ya utekelezaji wa mwaka 2019/2020 yanadhihirisha mchango wa MKURABITA na urasimishaji kwa ujumla katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu. Aidha, lengo la MKURABITA la kuwawezesha wananchi walio wengi wanaomiliki rasilimali na biashara katika sekta isiyo rasmi kuingia katika sekta rasmi linawiana vyema na malengo ya kitaifa yakiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) na Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2015.

Napenda kuishukuru kwa dhati Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Alli Mwinyi; Mawaziri wenye dhamana ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu; Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA na Viongozi wengine wa Sekta za Umma na Binafsi kwa miongozo, maelekezo na michango yenu wakati wote.

Kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Uongozi niendelee kutoa ahadi kwa watanzania wote juu ya nia yetu ya kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia wananchi wanaorasimisha rasilimali na biashara zao. Kamati itaendelea kushirikiana na wadau wa urasimishaji na wadau wa maendeleo ili kufikia lengo kuu la serikali la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Nitoe rai kwa wadau wote kuunga mkono utekelezaji wa MKURABITA kama sehemu ya jitihada za serikali katika kuwawezesha wananchi walio wengi kuwa washiriki katika kujenga uchumi endelevu.

Mhe. Balozi Daniel Ole Njoolay

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA

NENO KUTOKA KWA MRATIBU WA MPANGO

Mpango wa Kurasimisha rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ni Mpango wa serikali wenye lengo la kuwawezesha wananchi walio wengi wanaomiliki rasilimali na biashara katika sekta isiyo rasmi kuingia katika sekta rasmi ili kushiriki kikamilifu katika mfumo rasmi kupitia rasilimali na biashara zilizorasimishwa na hivyo kuboresha shughuli zao za kiuchumi, kupunguza umasikini wa kipato na kuongeza pato la taifa.

Katika mwaka 2019/2020, MKURABITA imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa MKURABITA 2014/2015 – 2018/2019 uliohuishwa hadi 2019/2020. Dira ya MKURABITA ni "**kuwa kitovu cha maarifa katika kuwezesha upatikanaji na ukuzaji wa mitaji kupitia rasilimali na biashara zilizorasimishwa**". Ili kufikia ndoto hii, MKURABITA inatumia mbinu ya "Kujenga uwezo wa wamiliki rasilimali na biashara zilizorasimishwa katika kupata na kukuza mitaji" yao na hivyo kuwa kichocheo cha ujenzi wa uchumi wa viwanda. Kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/2020 zimejikita katika kuwezesha upatikanaji na ukuaji wa mitaji kwa wamiliki wa rasilimali na wanaoendesha biashara zilizorasimishwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Utekelezaji umehusisha Wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka za serikali za mitaa; Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA); Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB); Wakala wa Usajili na Leseni (BRELA); Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO); Chama cha Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA); Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF); Benki za CRDB, NMB, TPB, Benki ya Akiba na Benki ya Watu wa Zanzibar; pamoja na vyombo vya habari Tanzania Bara na Zanzibar. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2019/2020 yameleta matumaini mapya ya kuendelea na utekelezaji kwa miaka mingine.

Nitoe shukrani za dhati kwa Ofisi ya Rais Ikulu inayoratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji, wizara zenye dhamana ya ardhi, Biashara, na wizara zinazohusika na serikali za mitaa Tanzania Bara na Zanzibar ambao ndiyo wadau wa kwanza katika utekelezaji. Nishukuru pia wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), na kwa namna ya pekee Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za mitaa kwa kutushauri na kutuelekeza bila kuchoka. Tunaahidi kuendelea kutekeleza ajenda hii kwa ufanisi na ubunifu zaidi utakaowezesha kuwafikia watanzania wengi zaidi.

CPA. Dkt. Seraphia Robert Mgembe
Mratibu wa Mpango

KAMATI YA UONGOZI WA MKURABITA

Kamati ya Uongozi ya MKURABITA ndiyo chombo cha juu chenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Mpango. Mwenyekiti wa Kamati huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati Wajumbe huteuliwa na Waziri mwenye dhamana na MKURABITA kwa kuzingatia uwakilishi wa Kisekta kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa MKURABITA, 2019/2020

Na.	Jina	Taasisi	Wadhifa
1	Balozi Daniel Ole Njoolay	Mwenyekiti, MKURABITA	Mwenyekiti
2	Immaculata Mwanja Senje	Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Upangaji na Usanifu wa Miji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Tanzania Bara	Makamu Mwenyekiti
3	Ened Munthali	Mratibu, Idara ya Sera na Mipango Ofisi ya Rais, Ikulu, Tanzania Bara	Mjumbe
4	Emmanuel Herman Mayeji	Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Sera na Mipango Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria, Tanzania Bara	Mjumbe
5	Ritta N. Magere,	Afisa Biashara Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, Tanzania Bara	Mjumbe
6	Haji Yakub Janabi	Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Nishati, Tanzania Bara	Mjumbe
7	Augustine Kungu Henry Ollal	Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Madini, Tanzania Bara	Mjumbe
8	Salhina Mwita Ameir,	Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Zanzibar	Mjumbe
9	Nana Rowland Mwanjisi	Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Zanzibar	Mjumbe
10	Angelista Kihaga	Mkurugenzi Msaidizi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Idara ya Serikali za Mitaa; Sehemu ya Utawala Bora na Utoaji Huduma,	Mjumbe
11	CPA. Dkt. Seraphia Mgembe	Mratibu wa Mpango MKURABITA	Katibu

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 MKURABITA Kwa Muhtasari

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Septemba, 2003 kwa Tamko la Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa. Utekelezaji wa MKURABITA ulianza rasmi Novemba 2004 Tanzania Bara na Zanzibar.

Azma ya Serikali ni kuwezesha watanzania wengi kushiriki katika fursa za uchumi kupitia rasilimali na biashara zilizorasimishwa.

1.2 Lengo la Kuanzishwa MKURABITA

Lengo la serikali kuanzisha MKURABITA ni kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na kuendesha biashara nje ya mfumo rasmi waweze kuzirasimisha na kuzitumia kupata mitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa unaondeshwa kwa mujibu wa sheria.

Uchumi wa kisasa, uchumi wa soko uliotanda duniani kote unaendeshwa kwa mikataba, kwa kukopa, kwa kuweka rehani na uaminifu wa kulipa

Hayati Benjamini William Mkapa,

Septemba 2003

1.3 Mantiki

Mantiki ya kuanzishwa MKURABITA imejengwa katika msingi wa umuhimu wa kuwawezesha wamiliki wa rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuingia katika mfumo rasmi. Kuingia kwao katika mfumo rasmi kutawawezesha kutumia rasilimali na biashara zilizorasimishwa kupata na kukuza mitaji ya shughuli zao za kiuchumi. Hali hii itachangia kupunguza umasikini wa kipato katika kaya, na hatimaye kuchangia kuinua uchumi wa taifa kwa ujumla.

Mageuzi ya uchumi na kuboresha uchumi mkuu peke yake haitoshi kupunguza umasikini, Maana umasikini ni kama pweza, Una mikia mingi. Kuboresha uchumi mkuu ni hatua ya kwanza tu katika safari ya kupunguza umaskini

Hayati Benjamini William Mkapa, 2003

1.4 Mchango wa MKURABITA katika Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa

Utekelezaji wa MKURABITA unazingatia Sera, Mikakati na Mipango ya kitaifa ambayo imechangia kuiwezesha Tanzania kufikia Uchumi wa kati. Mikakati na Mipango hiyo ni pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 (**NDV 2025)**, Mpango wa Pili waTaifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano(FYDP II), Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2004, na Ilani ya ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015. Kimataifa, utekelezaji umezingatia Ajenda ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs) na Ajenda ya Maendeleo ya Africa 2063.

1.4.1 MKURABITA na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

Malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Joseph Magufuli yameainishwa kwenye “NDV” 2025. Kati ya Mambo makuu matano ambayo ni mihimili ya NDV 2025, MKURABITA inachangia moja kwa moja katika mihimili miwili (2) ambayo ni Kuwezesha Maisha Bora pamoja na Uchumi wenye nguvu na shindani. Mchango wa MKURABITA kwenye Dira ya Taifa na Maendeleo umeoneshwa katika **Jedwali Na.1**

Jedwali Na. 1: MKURABITA katika Kufikia Malengo ya NDV 2025

Na.	Mihimili ya NDV 2025	Mchango wa MKURABITA
1	Kuwezesha Maisha Bora	kuwawezesha wamiliki wa rasilimali na biashara kuzirasimisha na kuzitumia kupata mitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa na hatimaye kuongeza kipato cha kaya na kupunguza umaskini
2	Uchumi wenye nguvu na shindani	Wananchi wengi wanaomiliki rasilimali na kuendesha biashara rasmi wanakuwa washiriki katika kukuza uchumi wa nchi unaotambulika kisheria.
		Mafunzo yanayotolewa kwa wamiliki wa rasilimali na biashara yanafanya mapinduzi ya kiuendeshaji na kiuzalishaji.
		Kuimarika kwa matumizi ya rasilimali na biashara zilizorasimishwa katika kupata mitaji kwenye taasisi za fedha kunachochea uwezo wa Wamiliki kufanya shughuli za kichumi ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

1.4.2 MKURABITA na Ilani ya CCM, 2015

Utekelezaji wa MKURABITA umezingatia Ilani ya CCM 2015 ambayo imeielekeza serikali kutekeleza mipango na mikakati inayolenga kuwawezesha wananchi wanyonge kiuchumi. Ibara ya 58 ya Ilani ya CCM 2015 imebainisha majukumu ya MKURABITA katika kuwawezesha wanyonge kiuchumi.

> Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ulianzishwa kwa lengo la kuwapa nguvu ya kiuchumi hasa wanyonge mijini na vijijini kwa kuwawezesha kumiliki ardhi na kufanya biashara katika mfumo rasmi wa kisasa unaoendeshwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo, kupitia urasimishaji rasilimali na biashara, MKURABITA ni nyenzo muhimu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kupunguza umaskini na kuongeza ajira nchini"
>
> *(Ilani ya CCM, 2015-2020)*

1.4.3 MKURABITA na FYDP II

Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II) ni muunganiko wa Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP I) na Mkakati wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). FYDP II umejengwa katika misingi mikuu mitatu ambayo ni uchumi wa viwanda, maendeleo ya watu na ufanisi wa utekelezaji. Vifungu 6.3.5 na 6.3.6 vya FYDP II vinatoa ufafanuzi wa mageuzi yatakayofanyika kuwezesha ufanisi kwenye urasimishaji ardhi na biashara katika kukuza uchumi. MKURABITA inachangia katika malengo yote matatu.



1.5 Awamu za Utekelezaji

Muundo wa utekelezaji wa MKURABITA umegawanyika katika awamu kuu Nne (4) ambazo ni Tathmini ya sekta isiyo rasmi, Maandalizi ya maboresho, Utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho pamoja na Ukuaji wa mitaji na utawala bora.



Kabla ya kuanza Awamu ya Kwanza ya Tathmini ya Sekta Isiyo Rasmi 2004, Hayati Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano aliwaeleza watanzania juu ya umuhimu wa kufanya tathmini.

> ***"Hatua inayofuata ni ya kutafiti hali halisi ya sekta isiyo rasmi nchini, kwa kuwa mipango yote ya maendeleo inahitaji takwimu. Hatuwezi kuwasaidia walio katika sekta isiyo rasmi kutumia rasilimali zao kupata, mitaji iwapo hatujui wana nini. Hatuwezi kubuni sheria, kanuni, na taratibu zitakazowarahisishia kuingia kwenye sekta rasmi iwapo hatujui mifumo na mitandao ya ufanyaji kazi, biashara, na mikataba wanayotumia katika sekta isiyo rasmi"***
>
> *Hayati Benjamini William Mkapa*

1.6 Dira na Dhima ya MKURABITA

MKURABITA imejiandaa kuwawezesha watanzania kufikia ndoto yao ya kuwa washiriki katika uchumi wa kati unaoendeshwa kwa misingi ya sheria. Dira ya MKURABITA ni "***Kuwa Kitovu Mahiri cha Kuwezesha Urasimishaji wa rasilimali ardhi na biashara kwa upatikanaji Mitaji***". Ili kufikia ndoto hii MKURABITA inatumia dhima ya "Kujenga uwezo wa wamiliki rasilimali na biashara zilizorasimishwa katika kupata na kukuza mitaji". Lengo la Serikali ilikuwa ni kuwawezesha wanufaika wa urasimishaji kupata mitaji na hivyo kuwa washiriki katika uchumi wa soko unaoendeshwa kwa misingi ya sheria.



1.7 Tunu za Msingi

Uwezo wa MKURABITA katika kutekeleza majukumu unawezeshwa na Tunu sita (6) za msingi ambazo ni **Uwajibikaji, Umoja, Uwazi, Uadilifu, Heshima, na Ubunifu.** Tunu hizi zinasimamia tabia na mienendo ya watumishi na wadau wa MKURABITA.

1.8 Wadau wa MKURABITA

MKURABITA inashirikiana na wadau mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar, zikiwemo Wizara zinazohusika na Ardhi; Biashara; TAMISEMI; Fedha na Mipango; Kilimo na Mifugo; Madini; Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi; Taasisi za Umma; Sekta Binafsi; Taasisi za Fedha; Vyombo vya Habari; Wadau wa Maendeleo na Wananchi/Wanufaika. Wadau hawa hupimwa kwa kuzingatia umuhimu na nguvu ya kushawishi wadau wengine kuwa washiriki wa shughuli za urasimishaji.

1.9 Mfumo wa utekelezaji/Uendeshaji

Utekelezaji wa MKURABITA umejengwa katika dhana ya uwezeshaji wa wananchi kwa mfumo wa elimu, ujuzi na uwezeshaji wa upatikanaji wa mitaji. Utekelezaji unafanyika kwa mfumo wa ushirikishwaji wa wananchi Tanzania Bara na Zanzibar kuanzia ngazi ya Majiji, Manispaa, Wilaya, Miji, Kata/Shehia, Mitaa/Vijiji na Vitongoji. Ili kuimarisha misingi ya ushirikishaji, MKURABITA imebuni mbinu ya kujenga uwezo wa kiutendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo na vifaa vya utekelezaji.

1.10 Mpangilio wa Taarifa

Sura ya Kwanza	Sura hii inatoa Utangulizi
Sura ya Pili	Sura hii inahusu utekelezaji na mafanikio ya urasimishaji rasilimali ardhi
Sura ya Tatu	Sura hii inahusu utekelezaji na mafanikio ya urasimishaji Biashara
Sura ya Nne	Sura hii inahusu ujengaji uwezo kwa wamiliki wa ardhi
Sura ya Tano	Sura hii inahusu utekelezaji wa huduma saidizi
Sura ya Sita	Sura hii inahusu matokeo ya urasimishaji
Sura ya Saba	Sura hii inahusu rasilimali watu na fedha

SURA YA PILI

UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA URASIMISHAJI RASILIMALI ARDHI

Urasimishaji wa rasilimali ardhi unahusisha uandaaji, usajili na utoaji wa Hati Miliki za ardhi Mijini na Vijijini na Ujenzi wa Masijala za ardhi za Vijiji Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2019/20, MKURABITA ilipanga kutekeleza shughuli za uandaaji na utoaji wa Hati Miliki za Kimila katika Halmashauri za Wilaya Sita (6) za Tanzania Bara; Ujenzi wa Masijala za ardhi za vijiji vitatu (3) vya Tanzania Bara; na uandaaji na utoaji wa hati katika wilaya tano (5) za Zanzibar. Hadi kufikia Juni 2020, utekelezaji wa urasimishaji ardhi vijijini umefanyika kwa asilimia 67 kwa Tanzania Bara. Upungufu wa kufikia lengo umetokana na ukosefu wa fedha pamoja na mabadiliko ya mfumo wa utekelezaji kwa kutumia Mfuko Endelevu wa Urasimishaji Ardhi. Maelezo kwa kila eneo la utekelezaji ni kama yanavyobainishwa kwenye vipengele Na. 2.1 hadi 2.4



2.1 Uandaaji na utoaji wa Hati Miliki.

Katika mwaka, 2019/2020 uandaaji wa Hati milki umefanyika katika maeneo ambayo upimaji wa ardhi ulikwishafanywa. Hivyo Uandaaji na utoaji wa Hati za Milki umeanza na hatua ya uhakiki ardhi, uandaaji, usajili na utoaji wa hati kwa wananchi Tanzania Bara na Zanzibar.

2.1.1 Uandaaji na Utoaji wa Hati Miliki za Kimila Tanzania Bara

Katika mwaka 2019/2020, MKURABITA ilipanga kufanya uhakiki wa mashamba 6,303 yaliyopimwa kwa ajili ya uandaaji na utoaji wa CCROs katika Halmashauri sita (6) za Wilaya za Mpwapwa, Moshi, Kibiti,Rufiji, Butiama, na Sikonge.

i) Uhakiki wa mashamba

Hadi kufikia Juni 2020, kati ya mashamba **6,303** yaliyopimwa, mashamba **3,860** sawa na asilimia 61 yalihakikiwa ikilinganishwa na mashamba **2,443** sawa na **asilimia 39** ambayo hayakuhakikiwa. Moja ya sababu za mashamba kutohakikiwa ni upungufu wa taarifa za wamiliki wa mashamba kutokana na wamiliki wengi kutojitokeza wakati wa kuhakiki mashamba yao.



Halmashauri ya Wilaya ya Butiama inaongoza kwa wamiliki waliojitokeza kuhakiki mashamba ambao ni **asilimia 92** ikifuatiwa na Halmashauri za Wilaya za Mpwapwa na Rufiji **asilimia 78**. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ina kiwango kidogo (**asilimia 28**) cha wananchi waliojitokeza kuhakiki mashamba yao. Maelezo Zaidi kwenye **Jedwali Na.2**

Jedwali Na. 2: Hali ya Uhakiki wa Mashamba 2019/2020

Na.	Wilaya	Idadi ya vijiji	Mashamba yaliyopimwa	Mashamba yaliyohakikiwa	Mashamba yasiyohakikiwa	Asilimia ya Mashamba yaliyo Uhakiki	Asilimia ya Mashamba yasiyohakikiwa
1	Mpwapwa	1	707	554	153	**78%**	**22%**
2	Moshi	2	2,108	1,109	999	**53%**	**47%**
3	Kibiti	4	1,121	593	528	**53%**	**47%**
4	Rufiji	2	449	351	98	**78%**	**22%**
5	Butiama	2	1,121	1,031	90	**92%**	**8%**
6	Sikonge	3	797	222	575	**28%**	**72%**
	Wastani	**14**	**6,303**	**3,860**	**2443**	**61%**	**39%**

Kazi ya uhakiki wa mashamba na uandaaji wa CCROs ilifanyika kwa ushirikiano mkubwa kati ya Maafisa ardhi wa Halmashauri husika, viongozi wa vijiji na wamiliki wa mashamba.

Wenyeviti wa vijiji vya Kindi Kati na Mikameni Ghona wakikamilisha uhakiki wa wamiliki wa mashamba yaliyorasimishwa kabla ya kumkabidhi Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kuandaa CCROs

ii) Uandaaji wa CCROs

Kati ya mashamba **3,860** yaliyohakikiwa, mashamba **2,742** sawa na **asilimia 71** yalikuwa na taarifa kamilifu na hivyo kuandaliwa hati. **Mashamba 1,118** sawa na **asilimia 29** yalikuwa na upungufu wa taarifa na hivyo hati zake hazikuandaliwa. Maelezo zadi kwenye **Jedwali Na.3**



Jedwali Na. 3: Taarifa ya Uhakiki na Uandaaji wa Hati Miliki za Kimila

Na.	Halmashauri za wilaya	Mashamba yaliyohakikiwa	Mashamba yenye mapungufu	Mashamba yenye taarifa timilifu	hati zilizoandaliwan akusajiliwa	Asilimia ya mashama yenye mapungufu	Asilimia ya mashama yenye taarifa timilifu
1	Mpwapwa	554	266	288	288	48%	52%
2	Moshi	1,109	-	1,109	1,109	0%	100%
3	Kibiti	593	128	465	465	22%	78%
4	Rufiji	351	208	143	143	59%	41%
5	Butiama	1,031	516	515	515	50%	50%
6	Sikonge	222	-	222	222	0%	100%
	Jumla	**3,860**	**1,118**	**2,742**	**2,742**	**29%**	**71%**

iii) Utoaji wa CCROs



Kilele cha zoezi la uhakiki na uandaaji wa CCROs ni utoaji wa CCROs kwa wamiliki wa mashamba ili waweze kuzitumia kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo toka katika taasisi za fedha. Katika mwaka 2019/2020, jumla ya CCROs 2,742 zimetolewa kwa wamiliki. Kazi ya utoaji CCROs kwa wamiliki imekuwa iikifanywa kwa mfumo shirikishi na kwa njia ya mikutano ya hadhara ya wananchi na viongozi ili kutoa hamasa kwa wananchi kushiriki katika urasimishaji.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Kpt. (Mst.) George H. Mkuchika akikabidhi CCROs kwa Ndg. Yohana Yaredi Magoile, mkazi wa Kijiji cha Inzomvu, Wilaya ya Mpawapwa

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Kpt. (Mst.) George H. Mkuchika, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Inzomvu, Mpwapwa baada yakukabidhiwa CCROs zao.

iv) Umiliki wa ardhi kwa jinsi

MKURABITA kama chombo cha serikali ina wajibu wa kuhamasisha wanawake kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwemo umiliki wa mashamba na rasilimali nyingine. Kati ya hati 2,742 zilizoandaliwa na kutolewa, umiliki wa wanawake ni asilimia 20.4 tu ikiacha wanaume wakiwa na umiliki wa asilimia 77.2 na umiliki wa pamoja asilimia 2.5.

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji inaongoza kwa umiliki wa wanawake ambao ni asilimia 27 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Butiama yenye umiliki wa asilimia 26. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ni ya mwisho kwa umiliki wa wanawake ambao ni asilimia 9. Maelezo ya zaidi kwenye Jedwali Na.4

Mmoja wa wananchi wa kijiji cha Mahama Wilayani Chamwino mkoani Dodoma Bi. Grace Mfereji akikabidhiwa CCRO na Mbunge wa Jimbo la Chilonwa Mhe. Joel Mwaka wakati wa hafla ya kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima zaidi ya 100 wa kijiji hicho.

Jedwali Na. 4: Hali ya Umiliki wa mashamba kwa jinsi

Na.	Halmashauri ya wilaya	Hali ya umiliki wa mashamba yenye CCROs kwa Jinsi na kwa idadi				Hali ya Umiliki wa mashamba yenye CCROs kwa jinsi na kwa Asilimia		
		Wanaume	Wanawake	Ubia	Jumla	Wanaume	Wanawake	Ubia
1	Mpwapwa	232	56	0	288	81%	19%	0%
2	Moshi	894	215	0	1109	81%	19%	0%
3	Kibiti	350	94	21	465	75.3%	20%	4.7%
4	Rufiji	98	38	7	143	68.5%	27%	4.5%
5	Butiama	350	135	30	515	68%	26%	6%
6	Sikonge	192	20	10	222	86.4%	9%	4.6
	JUMLA	**2116**	**558**	**68**	**2742**	77.2%	20%	2.8%

2.1.2 Urasimishaji wa Ardhi Mjini

MKURABITA ilipanga kutekeleza urasimishaji katika Manispaa ya Iringa kwa kutumia dhana ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji ambao uliziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukopa fedha kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya urasimishaji. **Viwanja 1,000** vilipangwa kurasimishwa kama mradi wa mfano kabla ya kuendelea na urasimishaji katika maeneo mengine nchini. Hadi kufikia Juni 2020, utekelezaji umefanyika kwa asilimia **45.9** ambapo viwanja **459** vimerasimishwa kati ya **1,000** vilivyopangwa. Kiwango kidogo cha utekelezaji kimetokana na mabadiliko ya mfumo wa utekelezaji kwa kutumia mfuko endelevu wa Urasimshaji ambapo Serikali ilisitisha mfumo wa Halmashauri kukopa fedha kwenye benki za biashara.



2.1.3 Uandaaji na Utoaji wa Hati za Haki za Matumizi ya ardhi Zanzibar

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilitenga fedha kwa ajili ya kuendeleza shughuli za urasimishaji ardhi jambo ambalo linadhihirisha uendelevu wa utekelezaji wa ajenda ya urasimishaji kwa upande wa Zanzibar. **Viwanja 8,271** vimepimwa katika wilaya tano (5) ambazo ni Mjini Unguja, Wete, Mkoani, Kaskazini A na Unguja. Kati ya viwanja hivyo, **Hati 708** sawa na **asilimia 8.6** ziliandaliwa na hati 63 sawa na **asilimia 8.9** zilitolewa kwa wananchi. Uwepo wa idadi ndogo ya hati zilizoandaliwa na kutolewa kwa wananchi kunasababishwa na wamiliki wa ardhi kutokujitokeza wakati wa maandalizi ya hati. Sababu za kutojitokeza ni ukosefu wa viambatisho vya uthibisho wa



umiliki kwa kuwa asilimia kubwa ya umiliki unatokana na mirathi. Hati zilizoandaliwa na kutolewa zimeoneshwa kwenye Jedwali Na.5

Jedwali Na. 5: Hali, uandaaji na utoaji wa hati za Viwanja Zanzibar, 2019/2020

Na.	Wilaya/Shehia	Viwanja vilivyopimwa	Hati zilizoandaliwa	Hati zilizotolewa	Asilimia ya Hati zilizoandaliwa	Asilimia ya Hati zilizotolewa
1.	Mjini Unguja (Welezo)	2600	0	0	0.0%	0.0%
2.	Mjini Unguja (Jang'ombe)	907	349	44	38.5%	12.6%
3.	Wete (Limbani)	1300	195	12	15.0%	6.2%
4.	Mkoani (Chokocho)	469	70	0	14.9%	0.0%
5.	Unguja Kati (Chwaka)	1045	9	1	0.9%	11.1%
6.	Kaskazini A (Nungwi)	1300	38	4	2.9%	10.5%
7.	Wete (Kiungoni)	650	47	2	7.2%	4.3%
	Jumla	**8,271**	**708**	**63**	8.6%	8.9%

Zoezi la utoaji wa Hati za Haki ya Matumizi ya ardhi kwa wamiliki wa ardhi ni zoezi shirikishi ambalo llinajumuisha wananchi na viongozi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA, Mhe. Balozi Daniel Ole Njoolay, akiwa katika picha ya pamoja na wanufaika wa Urasimishaji Ardhi wa Shehia ya Jang'ombe Zanzibar wakati wa hafla fupi ya kukabidhi Hati kwa Wananchi

2.2 Ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji

Uwepo wa Masjala za Ardhi za Vijiji ni hitaji la kisheria katika mchakato wa urasimishaji wa ardhi vijijini. Katika mwaka 2019/2020, Jumla ya Shilingi. **128,247,340/=** zimetumwa katika Halmashauri za Wilaya ya Nachingwea **(24,116,440/=);** Mbarali **(44,173,000/=);** na Mpwapwa **(59,957,900/=)** kwa ajili ya ujenzi wa masjala.



Hadi kufikia Juni 2020, wastani wa utekelezaji wa kazi zilizopangwa za ujenzi wa masijala ni **asilimia 73**. Utekelezaji katika Kijiji cha Kapyo cha Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ni **asilimia 90** ya kazi ya ukamilishaji boma; Kijiji cha Mbondo Wilaya ya Nachingwea ni **asilimia 62** ya kazi ya ukamilishaji wa jengo na choo na Kijiji cha Inzomvu Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ni **asilimia 68** ya ukamilishaji wa boma.

Hatua ya ujenzi wa Masjala ya Kijiji cha Mbondo Nachingwea

Hatua ya ujenzi wa masjala ya Kijiji cha Inzomvu Mpwapwa

Hatua ya ujenzi wa masjala ya Kijiji cha Kapyo Mbarali

SEHEMU YA TATU

UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA URASIMISHAJI BIASHARA

Urasimishaji na Uendelezaji Biashara ni kati ya majukumu muhimu ya MKURABITA. Katika mwaka 2019/2020 shughuli za urasimishaji na uendelezaji wa biashara zimehushisha Kujenga Uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara, Kutoa mafunzo kwa wamiliki wa biashara, Usajili wa biashara na kufanya Utafiti wa Msingi. Shughuli hizi zimefanyika kwa wastani wa **asilimia 72** kwa Tanzania Bara na **asilimia 57** kwa upande wa Zanzibar. Maeneo yaliyohusika ni Halmashauri ya Jiji la Mwanza; Manispaa za Songea na Tabora; pamoja na Halmashauri za Miji ya Babati na Kahama kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar shughuli za Urasimishaji na uendelezaji biashara zimefanyika katika wilaya za Mjini, Magharibi B na Wete.



3.1 Kujenga Uwezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara

MKURABITA ilipanga kujenga uwezo wa utekelezaji wa urasimishaji na uendelezaji wa biashara katika Mamlaka tano (5) za Serikali za Mitaa. Utekelezaji umefanyika kwa wastani wa **asilimia 95.8** na ulihusisha kutoa mafunzo kwa wadau wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara; Kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara pamoja na Kutoa vifaa vya utekelezaji wa urasimishaji biashara.



3.1.1 Kutoa Mafunzo kwa Wadau wa Urasimishaji

Mafunzo ya kujenga uwezo wa kiutendaji kwa ajili ya urasimishaji biashara yalifanyika katika Jiji la Mwanza, Manispaa za Songea na Tabora pamoja na Halmashauri za Miji ya Babati na Kahama. Lengo la mafunzo lilikuwa ni kuhamasisha wadau kushiriki katika utekelezaji wa urasimiahaji biashara katika Vituo vilivyoanzishwa. Wadau katika utekelezaji ni pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, TRA, SIDO, NSSF, TCCIA na Benki za Biashara ambapo mahudhurio ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.6.**

Na.	**Wadau**	**Halmashauri**					**Jumla**
		Babati	**Kahama**	**Tabora**	**Songea**	**Mwanza**	
1	Halmashauri	2	2	2	2	2	10
2	Benki ya CRDB	1	1	1	1	1	5
3	Benki ya NMB	1	1	1	1	2	6
4	SIDO	1	0	1	1	2	5
5	TCCIA	1	1	2	1	1	6
6	TRA	1	1	1	1	1	5
7	NSSF	1	1	1	1	1	5
8	TANTRADE	1	0	0	0	0	1
	Jumla	**9**	**7**	**9**	**8**	**10**	**43**
	Matarajio	**8**	**8**	**8**	**8**	**8**	**40**
	Asilimia ya utekelezaji	**112.5**	**87.5**	**112.5**	**100**	**125**	**107.5**

3.1.2 Kutoa fedha kwa ajili ya uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara.

Jumla ya shilingi **106,123,080/=** zilitolewa kwa ajili ya ukarabati wa majengo yaliyoainishwa na kwa ajili ya uanzishwaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Wilaya ya Nyamagana), Manispaa za Songea na Tabora pamoja na Halmashauri za Miji ya Babati na Kahama kwa Tanzania Bara na Wilaya ya Mjini Unguja kwa upande wa Zanzibar.

3.1.3 Kutoa Vifaa katika Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara

Ili kurahisisha shughuli za urasimishaji na uendelezaji wa biashara, Halmashauri zimejengewa uwezo kwa kupewa vifaa ambavyo ni kompyuta moja (1), 'Printer' moja (1), 'UPS' moja (1) na 'Scanner' moja (1) kwa kila Kituo kilichoanzishwa. Utoaji wa vifaa umefanyika kwa asilimia 80 Tanzania Bara na asilimia 100 kwa Zanzibar . **Jedwali 7**.

Jedwali Na. 6: Utoaji wa Vifaa vya urasimishaji Biashara Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/2020

Na.	Halmashauri	Kompyuta	Printa	UPS	Skana
	Tanzania Bara				
	Babati	1	1	1	1
	Kahama	1	1	1	1
	Tabora	1	1	1	1
	Songea	0	0	0	0
	Nyamagana	1	1	1	1
	Jumla	**4**	**4**	**4**	**4**
	Lengo	**5**	**5**	**5**	**5**
	Wastani (Tanzania Bara)	**80%**	**80%**	**80%**	**80%**
	Zanzibar				
	Mjini	1	1	1	1
	Jumla	**1**	**1**	**1**	**1**
	Lengo	**1**	**1**	**1**	**1**
	Wastani (Zanzibar)	**100%**	**100%**	**100%**	**100%**

NB: "Vifaa kwa ajili ya Manispaa ya Songea vitatolewa mara baada ya kituo cha urasimishaji na uendelezaji biashara kukamilika".

3.2 Uanzishaji wa Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara

MKURABITA kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Zanzibar ilipanga kuanzisha Vituo Jumuishi sita (6) vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara ambapo Tanzania Bara (5) na Zanzibar (1). Lengo la Vituo hivi ni kurahisisha mchakato wa urasimishaji na uendelezaji biashara kufanyika kwa haraka na gharama nafuu.

"Uanzishwaji wa Vituo vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika halmashauri zetu ni sehemu ya ubunifu wa MKURABITA katika kutekeleza Mpango wa uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (BLUE PRINT 2018)"

Hadi kufikia Juni 2020, Vituo **vinne (4)** sawa na **asilimia 67** vimeanzishwa Tanzania Bara katika Halmashauri ya Jiji la, Manispaa ya Tabora, Halmashauri ya Mji wa Babati. Kwa upande wa Zanzibar Kituo kimoja (1) kimeanzishwa katika wilaya ya Mjini.

Muonekano wa mbele wa Jengo la Kituo Kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora

Muonekano wa mbele wa Jengo la Kituo Kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika wilaya ya Nyamagana (Jiji la Mwanza)

Muonekano wa mbele wa Jengo la Kituo Kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika Halmashauri ya Mji wa Babati

Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara Wilaya ya Mjini (Unguja)

3.3 Mafunzo ya urasimishaji kwa wamiliki wa Biashara

Mafunzo ya urasimishaji biashara yalipangwa kufanyika kwa wafanyabiashara **5,000** Tanzania Bara katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Wilaya ya Nyamagana); Manispaa ya Songea na Tabora; Halmashauri ya Miji ya Kahama na Babati. Katika utekelezaji. Wafanyabiashara **1,529** sawa na **asilimia 31** walipata mafunzo katika Manispaa ya Tabora **(769)** na



Halmashauri ya Mji Babati **(760).** Utekelezaji umefanyika kwa kiwango kidogo kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19. Shughuli za mafunzo hazikufanyika katika Halmashauri za Jiji la Mwanza; Manispaa ya Songea na Mji wa Kahama.Kwa upande wa Zanzibar mafunzo yalipangwa kutolewa kwa Wafanyabiashara **240** katika Wilaya ya Magharibi B **(160)** na Wilaya ya Wete **(80).** Hadi kufikia Juni 2020, mafunzo yametolewa kwa wamiliki wa biashara **210** sawa na asilimia **91** ambapo Wilaya ya Magharibi B **(130)** na Wilaya ya Wete **(80)**. Maelezo zaidi kwenye Jedwali Na.8

Jedwali Na. 7: Wamiliki wa biashara waliopata mafunzo Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/2020

Halmashauri/Wilaya	Wamiliki wa Biashara		Utekelezaji
	Lengo	**Utekelezaji**	
Tanzania Bara			
Mwanza	1,000	0	0%
Songea	1,000	0	0%
Tabora	1,000	769	77%
Kahama	1,000	0	0%
Babati	1,000	760	76%
Wastani(Tanzania Bara)	**5,000**	**1529**	**31%**
Zanzibar			
Mjini Magharibi	160	130	81%
Wete	80	80	100%
Wastani (Zanzibar)	**240**	**210**	**91%**

3.4 Usajili wa biashara

Usajili wa biashara ulipangwa kufanyika kwa wafanyabiashara **5,000** Tanzania Bara katika Halmashauri za Jiji la Mwanza; Manispaa za Songea na Tabora; na Miji ya Kahama na Babati.



Hadi kufikia Juni 2020, Wafanyabiashara **3,274** sawa na **asilimia 65** walisajili biashara Tanzania Bara katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza (Nyamagana) (537); Manispaa za Songea (385) na Tabora (1,028); Halmashauri za Miji ya Babati (500) na Kahama (824). Utekelezaji umefanyika kwa kiwango kidogo kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa COVID 19. Kwa upande wa Zanzibar usajili wa biashara ulipangwa

kufanyika kwa biashara **240** katika Wilaya ya Magharibi B **(160)** na Wilaya ya Wete **(80).** Hadi kufikia Juni 2020, usajili umefanyika kwa biashara **65** sawa na asilimia **27** ambapo Wilaya ya Magharibi B biashara **45** zimesajiliwa na Wilaya ya Wete biashara zilizosajiliwa ni **20.** Maelezo zaidi kwenye Jedwali Na. 9

Jedwali Na. 8: Usajili wa Biashara Tanzania Bara na Zanzibar, 2019/2020

Halmashauri	Biashara zilizosajiliwa		Asilimia ya Utekelezaji
	Lengo	**Utekelezaji**	
Tanzania Bara			
Mwanza	1,000	537	54%
Songea	1,000	385	39%
Tabora	1,000	1,028	103%
Kahama	1,000	824	82%
Babati	1,000	500	50%
Wastani(Tanzania Bara)	**5,000**	**3,274**	**65%**
Zanzibar			
Mjini Magharibi	160	45	28%
Wete	80	20	25%
Wastani (Zanzibar)	**240**	**65**	**27%**

3.5 Utafiti wa Msingi

Utafiti wa Msingi hufanyika kabla ya kuanza mchakato wa urasimishaji wa biashara kwa lengo la kutambua hali halisi ya biashara na mahitaji ya wafanyabiashara. Kulingana na matokeo ya utafiti wa msingi mpango kazi uliandaliwa ili kuanza urasimishaji. Wastani wa utekelezaji ni 103% ambapo Halmashauri ya mji wa Kahama (113%) iko juu ya wastani. Hii ni kutokana na kuhamasika kwa wafanyabiashara wa Mji wa Kahama kutaka kurasimisha biashara zao. Aidha, Uongozi wa Halmashauri ya Kahama umemiliki zoezi kwa asilimia 100. Utafiti wa msingi umefanyika katika Halmashauri za Jiji la Mwanza; Manispaa za Songea na Tabora; na Miji ya Kahama na Babati. Ukusanyaji wa taarifa uwandani ulizingatia matumizi ya mbinu za kisasa za utafiti wa msingi ambapo



takwimu za biashara zilikusanywa kwa mfumo wa TEHAMA. Utafiti wa msingi umehusisha wafanyabiashara 5,165 sawa na asilimia 103.2.

Tathmini ya Utafiti wa Msingi kwa wafanyabiashara katika Halmashauri za Jiji la Mwanza (Wilaya ya Nyamagana); Manispaa za Songea na Tabora; Miji ya Kahama na Babati ulifanyika ili kubaini hali za wafanyabiashara katika umiliki wa biashara, mauzo, ulipaji kodi, mitaji na vyanzo vyake; uhitaji wa mafunzo; taarifa binafsi; ajira na upatikanaji wa mikopo. Kipengele namba (i) hadi (vi) ni maelezo ya kina ya matokeo ya uchambuzi wa utafiti wa msingi:-

i) Hali ya Umiliki wa Biashara kwa aina ya umiliki

Hali ya umiliki wa biashara kwa asilimia inaonesha kuwa kwa wastani asilimia 96 ya wafanya biashara wanamiliki biashara binafsi ukilinganisha na asilimia 3 wanaoendesha kwa ubia. Waliosajili makampuni ni asilimia 1 tu katika maeneo yote.



ii) Hali ya Umiliki wa biashara kwa umri

Kwa wastani asilimia 52 ya wamiliki wa biashara ni vijana wa umri kati ya miaka 18-35 ikifuatiwa na asilimia 31 wenye umri kati ya miaka 36-44. Wafanyabiashara wenye zaidi ya miaka 60 ni asilimia 2. Hivyo ni dhahiri kwamba lipo kundi kubwa la watanzania vijana wanaoendesha shughuli za kiuchumi.



iii) Hali ya Umiliki wa Biashara kwa Jinsi

Kwa wastani, sehemu kubwa ya wamiliki wa biashara sawa na asilimia 58 ni wanaume ikilinganishwa na wanawake asilimia 42. Halmashauri ya Mji wa Kahama inaongoza kwa umiliki wa wanaume ambao ni asilimia 64 ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa asilimia 63. Wastani wa umiliki wa biashara kwa wanaume na wanawake katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea ni asilimia 50 kwa 50.



iv) Usajili wa Biashara (BRELA, TRA na Leseni)

Jumla ya biashara 399 zimesajiliwa BRELA, biashara 3,274 zimesajili Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) katika Halmashauri za Jiji la Mwanza; Manispaa ya Songea na Tabora; na Miji ya Kahama na Babati.



v) Hali ya Utunzaji Kumbukumbu za Biashara, Akaunti za Benki na Upatikanaji wa Mikopo

Maelezo katika kipengele (a) – (c) yameonesha hali ya utunzaji wa kumbukumbu, Akaunti za benki na upatikanaji wa mikopo kama ifuatavyo:-

a) Kwa wastani asilimia 53 ya wafanya biashara hawatunzi kumbukumbu za biashara. Halmashauri ya Manispaa ya Songea inaongoza kwa kuwa na wafanyabiashara wengi wasiotunza kumbukumbu za biashara ambao ni asilimia 57.



b) Asilimia 34 ya biashara zilizofanyiwa tathmini zinamiliki akaunti za benki ikiongozwa na wamiliki wa biashara wa Halmashauri ya Mji wa Babati kwa asilimia 25.



c) Kwa wastani ni asilimia 19 ya biashara zilizofanyiwa tathmini zimekopa mikopo katika taasisi za fedha ikiogozwa na wamiliki wa biaashara wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea ambao ni asilimia 28



vi) Hali ya Upatikanaji wa mitaji ya kuanzia



Ukuaji wa mitaji unategemea pia chanzo cha mtaji. Hali ya upatikanaji wa mitaji kwa maeneo yote yaliyofanyiwa tathmini inaonesha kuwa wamiliki wa biashara sawa na asilimia 86.8 wanapata mitaji ya kuanzia biashara kwa fedha zao wenyewe. Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Manispaa ya Tabora zinaongoza kwa kuwa na asilimia 90 ya wafanyabiashara walioanza na mitaji binafsi ikifuatiwa na Halmashauri ya Mji wa Kahama wenye asilimia 87. Tathmini imeonesha pia, asilimia 1.8 wametumia mfuko wa vijana na wanawake kupata mitaji ambapo ikiongozwa na Halmashauri ya Mji wa Babati (asilimia 6). Maelezo zaidi kwenye **Jedwali Na. 10**

Jedwali Na. 9: Hali ya Vyanzo vya Mitaji kwa asilimia

Chanzo cha Mtaji	Songea	Mwanza	Kahama	Babati	Tabora	Wastani
Pesa yako mwenyewe	**86**	**90**	**87**	**81**	**90**	**86.8%**
Mali ya kuazima	**0**	**2**	**5**	**3**	**2**	**2.4%**
Benki za Biashara	**6**	**3**	**4**	**2**	**1**	**3.2%**
Taasisi ndogo za kifedha	**4**	**3**	**2**	**1**	**1**	**2.2%**
zawadi	**4**	**2**	**1**	**4**	**0**	**2.2%**
Mifuko ya vijana na wanawake	**0**	**0**	**1**	**6**	**2**	**1.8%**
Chanzo kingine (Kilimo)	**0**	**0**	**0**	**3**	**4**	**1.4%**
Jumla/idadi	**1,113**	**1,138**	**1,258**	**1,142**	**1,128**	**100%**

SURA YA NNE

KUJENGEA UWEZO WAMILIKI WA ARDHI NA BIASHARA

Urasimishaji unalenga kutoa suluhisho la kipekee la rasilimali za wananchi kutokutambulika kisheria na kuendelea kuwa mfu na hivyo kutoweza kutumika katika kupata na kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi. Baada ya kurasimisha ardhi na biashara wamiliki wake hujengewa uwezo wa kuzitumia kupata na kukuza mitaji ya shughuli zao za kiuchumi.

Sehemu ya wakulima wa Kijiji cha Mahama Wilayani Chamwino wakifuatilia mafunzo ya kuwajengea uwezo ili waweze kuongeza tija katika uzalishaji baada ya mafunzo yaliyoendeshwa na Ofisi ya Rais, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Bw. Athmani Masasi akiwa kwenye picha ya pamoja na sehemu ya wakulima walioshiriki katika mafunzo yakuwajengea uwezo ili waweze kuzalisha kwa tija.

Kaimu Mkurugenzi wa Urasimishaji Rasilimali na Biashara akiongea na waandishi wa Habari baada kuhitimisha mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa Mtwara

Wafanya biashara wa Mtwara wakiwa kwenye picha ya Pamoja baada ya kuhitimu mafunzo ya kujengewa uwezo wa uendeshaji biashara na MKURABITA

Utekelezaji unafanyika kwa kutoa mafunzo kwa wamiliki wa ardhi ya namna ya kutumia hati miliki kupata mikopo katika Taasisi za fedha. Wamiliki wa biashara pia hupewa mafunzo ya uendelezaji biashara ili waweze kupata mitaji ya kukuza biashara zao. Mafunzo haya hutolewa kwa kushirikiana na wadau mbalimabli wa sekta za Umma na Binafsi Tanzania Bara na Zanzibar ambao ni Mamlaka za Serikali za Mitaa, TRA, ZRB, BRELA, PBRA, TANTRADE, SIDO,SMIDA, NSSSF, PSSSF, Taasisi za Fedha na AMCOS.

Maafisa kutoka NSSF na SIDO wakitoa mada kuhusu urasimishaji biashara - Geita

4.1 Mafunzo ya kutumia Hati Miliki kupata Mikopo

Wakulima waliorasimisha mashamba na kupata CCROs hupewa mafunzo ya namna ya kuzitumia kupata mitaji katika Taasisi za fedha. Mafunzo yalipangwa kufanyika kwa wakulima 200 na Viongozi 20 wa Vyama vya Wakulima wa Vijiji vya Mvumi na Magubike katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Mafunzo yalifanyika katika Halmashauri ya Kilosa tu kutokana na ugonjwa wa COVID 19 ambao uliathiri mikusanyiko ya watu. Hadi kufikia Juni 2020, mafunzo yametolewa kwa wakulima 180 sawa na asilimia 90 na Viongozi 22 wa Vyama vya Wakulima sawa na asilimia 110. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Jedwali Na. 11**

Jedwali Na. 10: Idadi ya Wakulima na Viongozi waliopata mafunzo ya kujenga uwezo 2018/2020

Na.	Kijiji	Wakulima	Me	Ke	Viongozi	Me	Ke	Vikundi
1.	Magubike	103	76	27	12	7	5	10
2.	Mvumi/Gongwe	77	48	29	10	6	4	8
	Jumla	**180**	**124**	**56**	**22**	**13**	**9**	**18**
	Asilimia		**69**	**31**		**59**	**41**	

4.2 Ushiriki wa wanawake kwenye mafunzo

Ushiriki wa wakulima na viongozi wa wakulima kwenye mafunzo unaonesha kuwa, ushiriki wa wanawake ni mdogo ikilinganishwa na wanaume. Wastani wa wanawake walioshiriki mafunzo ya wakulima ni asilimia **31** na viongozi ni asilimia **41**. Hali hii inaonesha kuwa wanawake wanaomiliki rasilimali ardhi zilizorasimishwa ni wachache ikilinganishwa na wanaume.



4.3 Mafunzo ya Uendelezaji Biashara

Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara vinalenga kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma za uendelezaji wa biashara kwa haraka na gharama nafuu katika eneo linalotoa huduma za urasimishaji sehemu moja. MKURABITA kwa kushirikiana na wadau wengine hutumia Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na uendelezaji wa biashara kutoa mafunzo ya uendelezaji wa biashara kwa wafanyabiashara waliorasimisha biashara zao. Wadau wanaoshirikiana na MKURABITA ni Mamlaka za Serikali za Mitaa, TRA, ZRB, BRELA, BPRA, TANTRADE, SIDO,SMIDA, NSSF, PSSSF na Taasisi za Fedha.

Mafunzo yanayotolewa yanahusisha elimu ya fedha na upatikanaji wa Mikopo, huduma atamizi, upatikanaji wa masoko, pamoja na Mipango ya biashara na uwekezaji.

Katika mwaka 2019/20 Mafunzo yalipangwa kutolewa kwa wafanyabiashara katika Vituo vilivyoanzishwa kwenye Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Manispaa za Tabora, Halmashauri za Mji wa Babati na Kahama kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar mafunzo yalipangwa kutolewa katika Kituo kilichoanzishwa Wilaya ya Mjini.

Hadi kufikia Juni, 2020, mafunzo ya uendelezaji biashara hayakuweza kufanyika kutokana na ugonjwa wa COVID 19 ambao uliathiri mikusanyiko ya watu. Katika hatua nyingine ya utekelezaji, MKURABITA imekubalina na Benki ya NMB kuwawezesha wafanyabiashara 50 waliorasimisha biashara katika kila Halmashauri Tanzania Bara na Zanzibar kujiunga na Klabu za Biashara za benki ya NMB. Klabu hizi zinatoa fursa kwa wafanyabiashara kuunganishwa na mtandao wa wafanyabiashara ambao ni wateja na NMB, kupata elimu ya usimamizi wa fedha, kutoa maoni ya wateja na kushiriki katika majukwaa yanayoandaliwa na benki hiyo.

SURA YA TANO

UTEKELEZAJI NA MAFANIKIO YA HUDUMA SAIDIZI

Huduma saidizi ni shughuli ambazo zinawezesha kufikiwa kwa malengo yanayotokana na shughuli za msingi ambazo ni urasimishaji wa rasilimali na biashara. Ufanisi wa utekelezaji wa urasimishaji ardhi na biashara unachangiwa na utekelezaji wa huduma saidizi. Katika mwaka 2019/2020 huduma saidizi ambazo zimetoa mchango mkubwa wa kuwezesha utekelezaji wa huduma za msingi za MKURABITA ni pamoja na Habari na Mawasiliano kwa Umma; Uratibu wa Mapendekezo ya Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi; pamoja na Ufuatiliaji na tathmini.

5.1 Habari na Mawasiliano



Utoaji wa Habari na mawasiliano kwa umma wa watanzania una mchango mkubwa sana wa kuwezesha shughuli za urasimishaji kufanyika kwa ufanisi na kwa gharama nafuu. Katika mwaka 2019/2020, MKURABITA imeendelea na utoaji wa elimu na habari kwa umma ili kujenga uelewa na kuwezesha wadau wengi zaidi kufahamu na kushiriki utekelezaji wa kazi za urasimishaji ardhi na biashara. Shughuli zilizopangwa kufanyika ni kuandaa na kurusha vipindi 20 vya habari na elimu kwa umma, kushiriki mikutano ya RCCs na DCCs ili kuendelea kuhamasisha na kutoa uelewa kwa viongozi wa mikoa na wilaya, kufanya

uhamasishaji kupitia mabaraza ya madiwani katika Halmashauri tatu (3) pamoja na kufanya uhamasishaji katika matukio maalum zikiwemo ziara za vongozi katika maeneo saba (7).

Hadi kufikia Juni, 2020, utekelezaji umefanyika kwa wastani wa asilimia 128. Vipindi vilivyoandaliwa ni 25 na vilivyorushwa katika Radio na Runinga ni 80. Hii ni kufuatia mahusiano mazuri kati ya MKURABITA na vyombo vya Habari. Aidha, umuhimu wa utekelezaji wa urasimishaji kwa wananchi, umetoa msukumo kwa vyombo vya Habari kuchangia kwa kutoa vipindi vya ziada. MKURABITA ilipata vipindi vya ziada kutoka kwenye radio na runinga zilizorusha vipindi. Radio na Runinga zilizorusha vipindi ni TBC, ZBC, ITV, Star TV/RAF, Channel 10, Clouds Media, Azam TV, Tanga TV, Tanga City Tv, Iringa MTV, Mbeya FM Radio, SUA TV /Radio pamoja na Wapo Radio.

Vituo na mitandao ya kijamii pia imekuwa sehemu ya utekelezaji wa shughuli za utoaji elimu na mawasiliano kuhusu tija ya urasimishaji nchini. Baadhi ya vituo na mitandao iliyotangaza shughuli za MKURABITA ni MAELEZO TV, Habari leo Online Tv, Michuzi TV, na Global TV.

Kupitia maandalizi ya vipindi walengwa mbalimbali wametoa shuhuda juu ya faida za kiuchumi za urasimishaji ardhi kama inavyoonekana kwa baadhi ya mashuhuda katika wilaya ya Mbarali.

Paulinus Msigwa wa kiji cha Ubaruku anaishukuru serikali kwa kupitia MKURABITA kwa kupima mashamba yao ambayo yamekuwa mkombozi wa Maisha yao kutokana na mabenki kuwakopesha bila mgogoro wowote. Anasema kwamba wamekuwa wakilima bila tija kuanzia mwaka 2001 hadi 2010 walipopata taarifa za serikali kurasimisiha mashamba yao.

Mzee Haruna Ngolo mkulima wa Ubaruku Mbarali anasema alikubali kurasimisha shamba lake baada ya kupewa elimu ya faida za urasimishaji na anasema ni kweli ameziona faida za kurasimisha shamba lake la mpunga.

Ndugu George Mwaijobele Afisa Ardhi Halmashaur ya wilaya ya Mbarali akithibitisha juu ya kazi ya urasimishaji iliyofanywa na MKURABITA katika vijiji vya Kapyo na Mabadaga

5.2 Uratibu wa Mapendekezo ya Maboresho ya Kisheria na Kitaasisi

MKURABITA iliandaa mapendekezo ya maboresho ya Kisheria na Kitaasisi yenye lengo la kurahisisha na kuharakisha urasimishaji wa ardhi na biashara Tanzania Bara na Zanzibar. Mapendekezo haya yanatekelezwa na Wizara za Kisekta za Tanzania Bara na Zanzibar.



MKURABITA ina wajibu wa kufuatilia na kuratibu utekelezaji unaofanywa na wizara za kisekta. Katika Mwaka 2019/20 Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni kuwasilisha Mapendekezo ya Maboresho 26 ya ardhi na 14 ya biashara katika Wizara za Kisekta kwa ajili ya utekelezaji; kufuatilia utekelezaji na kupima matokeo ya utekelezaji. Kupitia uratibu uliofanywa imeonekana kuwa hadi kufikia Juni 2020, wastani wa utekelezaji wa Mapendekezo ya Maboresho ulifikia asilimia 70 kwa Tanzania Bara ambapo Mapendekezo ya Maboresho ya sheria za ardhi yaliyotekelezwa ni manne (4) na ya biashara ni matano (5).

TATHMINI NA UFUATILIAJI

Ufuatiliaji na tathmini umefanyika ili kupima ufanisi na matokeo ya utekelezaji wa urasimishaji kwa kipindi cha mwaka 2020/2021. Ufuatiliaji umefanyika kwa kuhusisha menejimenti ya MKURABITA kupitia kitengo cha ufuatiliaji na tathmini na ziara za Viongozi wa Kitaifa za kukagua utekelezaji na kutoa maelekezo ya kuboresha urasimishaji;

Tathmini

Tathmini iliyofanyika katika mwaka 2020/2021, ililenga kubainisha matokeo ya urasimishaji na uendelevu wa urasimishaji biashara katika Halmashauri ya Morogoro, Tanga, Mtwara, Singida, Babati, Korogwe, Mvumero, Chamwino, Serengeti na Magu;

Matokeo ya Tathmini ya Urasimishaji Biashara katika Halmashauri ya Manispaa Morogoro, Singida na Mtwara, Jiji la Tanga na Mji wa Babati:

Muhtasari wa matokeo ya tathmini ya uendelevu wa urasimishaji biashara iliyofanyoka kwa wafanyabiashara 1,540 waliopata mafunzo wakati wa urasimishaji biashara katika Halmashauri ya Manispaa Morogoro, Singida na Mtwara, Jiji la Tanga na Mji wa Babati. Mtokeo kwa jumla ni kama ifuatavyo:-

- Asilimia 64 ya wafanyabiashara waliofanyiwa tathmini wanatunza kumbukumbu za biashara. Kabla ya urasimishaji wafanyabiashara hawakuwa wanatunza kumbukumbu zozote za biashara zao;
- Asilimia 24 ya wafanyabiashara 1,540 wamefungua akaunti za benki;
- Kuongezeka kwa leseni za biashara kutoka leseni 10,380 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia leseni 13,769 kwa mwaka 2019/20
- Kuongezeka kwa mapato ya leseni kutoka TZS Milioni 660 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia TZS bilioni 1.75 kwa mwaka 2020/21;
- Biashara zimepanuka kutokana na kuendeshwa kitaalam na hivyo kutoa ajira takriban 1,008;

Matokeo ya Urasimishaji Ardhi katika Halmashauri za Wilaya ya Korogwe, Mvumero, Chamwino, Serengeti na Magu.

Muhtasari wa matokeo ya tathmini ya uendelevu wa urasimishaji wa ardhi iliyofanyika kwa wakulima 442 waliopata mafunzo wakatia wa urasimishaji, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe(120), Chamwino(75), Mvomero(66), Serengeti(70) na Magu(86). Matokeo ni kama ifuatavyo:-

- Ajira zilizotengenezwa kutokana na urasimishaji ni 646 ambapo wanaume ni asilimia 59 na wanawake ni asilimia 41;
- Halmashauri zimeendelea kutoa hati za kimila, ambapo jumla ya hati 11,936 kati ya 15,249 zimetolewa kwa wananchi;
- Ongezeko la umiliki wa akaunti za benki kutoka wastani wa asilimia 24 kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 35 kwa mwaka 2020/21;
- Wakulima wanaotunza kumbukumbu za kilimo wameongezeka kufikia asilimia 44 ikilinganishwa na awali ambapo wakulima walikua hawatunzi kumbukumbu; na
- Asilima 6 ya Wananchi wamekopa katika taasisi za fedha kiasi cha shs trillioni 1.856

5.3.2 Ziara za Viongozi za Kukagua Utekelezaji

Viongozi wenye dhamana ya kutoa miongozo, na maelekezo kwa MKURABITA, walifanya ziara za ukaguzi wa utekelezaji wa shughuli za urasimishaji ardhi na biashara nchini. Viongozi waliohusika katika ziara hiyo ni Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wenye dhamana na MKURABITA; Wajumbe wa Kamati za
Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA.

i. Mawaziri wenye Dhamana ya MKURABITA

Mhe**.** Kapt. (Mst). George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi**,** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mhe. Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora walifanya ziara tatu (3) za kukagua utekelezaji wa shughuli za MKURABITA katika Halmashauri za Wilaya ya Mpwapwa, Songwe, Rungwe, Mbarali na Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Wakati wa ziara viongozi walitoa Hati Miliki za Kimila kwa wananchi waliorasimisha ardhi zao na walihamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za urasimishaji. Vilevile, walitoa maelekezo kwa MKURABITA kuongeza kasi ya kurasimisha ardhi za wananchi ili wapate Hati miliki.

Mhe. Kapt. mstaafu George Mkuchika,Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora akiwa kwenye picha ya pamoja na wananchi wa kijiji cha Inzovu wilaya ya Mpwapwa waliopatiwa Hati za Hakimili za kimila katika Kijiji hicho baada ya kurasimisha mashamba yao.

ii. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ilifanya ziara moja (1) ya kukagua utekelezaji wa Uanzishwaji wa Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara katika Manispaa ya Singida.

Kamati ilitoa pongezi kwa MKURABITA kwa uamuzi wa kuanzisha Kituo Jumuishi cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika manispaa ya Singida kwa kuwa vimewawezesha wafanyabiashara kupata huduma kwa haraka na nafuu. Aidha, Kamati ilitoa maelekezo kwa Serikali kuendelea na utekelezaji wa kuanzisha Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji Biashara katika Halmashauri nyingine za Tanzania Bara na Zanzibar.

Afisa Biashara na Mratibu wa Kituo cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara Manispaa ya Singida Bw. Erick Sinkwembe akielezea shughuli na huduma zinazotolewa katika kituo hicho kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa walipotembelea kituo hicho.

Mfanyabiashara wa Manispaa ya Singida, Bi. Happy Francis akitoa maelezo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusiana na bidhaa anazozalisha wakati wa ziara ya kamati hiyo Mkoani Singida

iii. Ziara za Kamati ya Uongozi

Kamati ya Uongozi ilitembelea Zanzibar ili kukagua shughuli za urasimishaji kwa kipindi cha 2019/2020. Kamati ilikagua utekelezaji wa shughuli za MKURABITA ambazo zilikuwa ni kutembelea wajasiliamali mjini unguja na Kaskazini B; na kutembelea zoezi la utoaji wa hati kwa wamiliki wa ardhi katika Shehia ya Mpendae-Mkoa wa Unguja Mjini. Kamati ilitoa maelekezo kwa Menejimenti kuongeza kasi ya uandaaji na utoaji wa Hati za Matumizi ya Ardhi pamoja na mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara kutolewa kwa wafanyabiashara wengi zaidi.

Mfanyabiashara wa Mchele Visiwani Zanzibar (Zanzibar Rice)Yussuf Faki akitoa maelezo kwa baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya kamati hiyo kukagua shughuli wanazozifanya visiwani Zanzibar

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa MKURABITA Mhe. Balozi Balozi Daniel Ole Njoolay, akiwa katika picha ya pamoja na wanufaika wa Urasimishaji Ardhi wa Shehia ya Jang'ombe Zanzibar wakati wa hafla fupi ya kukabidhi Hati kwa Wananchi

SURA YA SITA

MATOKEO YA URASIMISHAJI

Utekelezaji wa urasimishaji ardhi na biashara umeleta manufaa kwa wananchi waliorasimisha rasilimali na biashara na kwa taifa. Wanufaika wa urasimishaji wamepata manufaa ya kujumuishwa kwenye huduma za kifedha, kupata mikopo kwenye taasisi za fedha, kupata ajira na ongezeko la usalama wa miliki. Aidha, uendelevu wa shughuli za urasimishaji na kupungua kwa migogoro ya ardhi kumeongeza uwezo wa wananchi kuzalisha zaidi. Manufaa ya kitaifa yaliyopatikana ni pamoja na ukuaji wa uchumi unaotokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na ada ya leseni; na kuongezeka kwa idadi ya walipa kodi kupitia kodi ya mapato.

6.1 Matokeo ya urasimishaji kwa wananchi

Urasimishaji umewezesha wanufaika kujumuishwa kwenye huduma za kifedha, kupata mikopo kwenye taasisi za fedha, ajira na ongezeko la usalama wa miliki.

6.1.1. Wanufaika kujumuishwa kwenye huduma za fedha

Wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara wameweza kufungua akaunti za benki katika benki mbalimbali Tanzania. Wanufaika hawa kwa sasa wamejumuishwa katika huduma za fedha na wanazitumia kuendesha shughuli zao.

Kwa mujibu wa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini ya mwaka 2020 **asilimia 69** ya wamiliki wa biashara katika Halmashauri ya Mji wa Njombe, asilimia **37** ya wamiliki wa ardhi katika Halmashauri ya wilaya ya Itigi na asilimia **78** ya wamiliki wa ardhi katika Halmashauri ya wilaya Mufindi wamefungua akaunti za benki.

6.1.2. Ongezeko la Utunzaji wa kumbukumbu

Kumekuwa na ongezeko la utunzaji wa kumbukumbu za biashara na kilimo kwa wamiliki wa ardhi na biashara waliorasimishwa. Kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya mwaka 2020 **a**silimia **69** ya wamiliki wa biashara katika Halmashauri ya Mji wa Njombe wanatunza kumbukumbu za biashara baada ya kupata mafunzo ya kutunza kumbukumbu. Kutunza kumbukumbu za biashara kumewawezesha wafanyabishara kuwa na vielelezo vya biashara zao ambavyo ni muhimu katika mchakato wa kuomba mkopo katika taasisi za fedha. Kumbukumbu pia zinamuwezesha mfanyabiashara kuwa na taarifa halisi za mapato na

matumizi ya shughuli zake ambazo zinaweza kutumika na mamlaka zingine kufanya maamuzi ikiwemo ukadiriaji wa kodi ya mapato. Kwa upande wa wakulima, kuna ongezeko la utunzaji wa kumbukumbu za kilimo ikilinganishwa na awali ambapo wakulima walikua hawatunzi kumbukumbu. Ufuatiliaji na tathmini ya mwaka 2020, imeonesha kuwa asilimia **98** ya wamiliki katika Halmashauri ya Mufindi wanatunza kumbukumbu za kilimo. Aidha, asilimia **96** ya wamiliki wa ardhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi wanatunza kumbukumbu za kilimo. Kumbukumbu zinamsaidia mkulima kujua mahitaji halisi ya kilimo chake ambazo zinamwezesha kujua gharama za kilimo kwa kuzingatia mbegu na pembejeo za kilimo. Pia kumbukumbu zinamsaidia katika kujua bei ya mauzo ya mazao yake ikilinganisha na bei za kitaifa na kimataifa.

6.1.3. Upatikanaji wa Mikopo ya wamiliki wa biashara

Urasimishaji umewezesha wamiliki wa biashara kuzitumia biashara zilizorasimishwa kupata mikopo kutoka taasisi za fedha. Wamiliki wa biashara katika Halmashauri tano (5) wameweza kukopa jumla ya **Shlingi. 4,010,000,000** kwa ajili ya mitaji ya kuendeshea biashara zao. Wamiliki waliokopa fedha hizi wapo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza, Manispaa za Songea na Tabora, Miji ya Babati na Kahama. Matokeo haya yanabainisha kuwa biashara zinaporasimishwa zinapata uwezo wa kukidhi vigezo vya mikopo katika taasisi za fedha.

Bw. Ngole Maduhu "…Nilipata mkopo kupitia mfuko wa vijana katika Halmashauri ya Mji Bariadi kwa ajili ya mashine ya kusaga…MKURABITA walipokuja kutoa mafunzo nilipata bahati ya kushiriki na kusaji biashara yangu kupitia kituo cha urasimishaji. baada ya kusajili fursa zilianza kufunguka Halmashauri ikanipatia zabuni ya kusambaza chakula kwenye baadhi ya shule za sekondari za bweni hali iliyonilazimu kwenda kukopa benki. Nawashukuru Wataalam wa biashara walioko kwenye Kituo cha Urasimishaji na uendelezaji biashara Bariadi ambao walinisaidia sana kuandaa mchanganuo na kuupeleka benki. Mtaji wangu umeongezeka naaminika na mabenki hata serikali kwa kuwa biashara yangu iko rasmi..."

6.1.4. Upatikanaji wa mikopo kwa Wamiliki wa ardhi

Urasimishaji umewezesha wamiliki wa ardhi kutumia CCROs kama dhamana kupata mikopo katika taasisi za fedha. Wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Itigi wametumia CCROs kama dhamana na kupata mikopo yenye thamani ya **Shilingi. 375,705,000.** Aidha, vyama vitano (5) vya wakulima vimedhaminiwa na AMCOS na kupata mikopo ya thamani ya shilingi **845,866,094.**

Bi. Ruhele Masaka, Meneja wa CRDB Tawi la Mbarali ambapo Wakulima wa Mbarali wameweza kunufaika na mkopo benki kupitia hati miliki za kimila kama dhamana. Pia kutokana na mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara yaliyotolewa na MKURABITA yamewezesha ongezeko la biashara zinazokopa.

Mzee Paulo Kasato kutoka Misungwi "…naishukuru sana MKURABITA, baada ya kuja hapa kijijini na kupima mashamba yetu wengi tulipata hati miliki na mafunzo kutoka kwa wataalam pamoja na mabenki walieleza kuwa tunaweza kukopeshwa hata matrekta kwa kutumia hizo hati, Mimi na ndugu yangu Jogori tulikwenda kukopa pesa na kununua trekta. Niliweza pia kununua ng'ombe na mbuzi pamoja na mashamba. Nilifanikiwa kurejesha mkopo wangu, sasa hivi najenga nyumba bora na ya kisasa…"

6.1.5. Upatikanaji wa Ajira

Urasimishaji umefungua fursa za ajira kwa kuwa unawezesha upatikanaji wa mitaji ambayo inaongeza wigo wa uzalishaji unaohitaji rasilimali watu ya kutosha. Utekelezaji wa mafunzo ya kuendesha kilimo biashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi umewawezesha wakulima kuendesha kilimo chenye tija na kuongeza fursa za ajira **478** katika mashamba ya chai.

Bw. Michael Kilagane anasema "Kupitia mafunzo ya KURABITA nimeweza kuongeza mtaji kwa kukopa benki na kuanzisha kiwanda kidogo cha kukamua alizeti iliyopelekea kutengeza ajira kwa vijana"

Agosti Matori, Mfanyabiashara Morogoro anasema "Kurasimisha biashara kumeniwezesha kupiga hatua ya kuanzisha kiwanda kidogo cha aluminium na kutengeneza ajira kwa baadhi ya watanzania"

6.1.6. Kuongezeka kwa Usalama wa miliki

Urasimishaji umeongeza thamani, usalama na uhakika kwa wamiliki kwa ardhi. Utoaji wa Hati Miliki kwa kila kipande cha ardhi iliyorasimishwa inaongeza usalama wa miliki kwa kuwa mmiliki wa ardhi anatambulika kisheria. Hati za Haki Milki za Kimila **1,631** zilizotolewa kwa wamiliki wa mashamba ya chai Mufindi, zimeongeza usalama na uhakika wa miliki kwa wananchi. Hili linathibitishwa na risala wananchi katika sherehe za utoaji wa hati katika maeneo mengi.

Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti (Mwenye sharti la mistari) na msaidizi wake wakiwa na hati wakisubiri kuzikabidhi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA Mhe. Balozi Mst. Daniel Ole Njoolay tayari kwa kuzitoa kwa wamiliki

Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi ya MKURABITA Mhe. Balozi Mst. Daniel Ole Njoolay akiwa na wananchi wa Kibiti baada ya kuwakabidhi Hati za Haki milki za kimila wilayani Kibiti

6.2 Matokeo ya Urasimishaji kwa Taifa

Urasimishaji umeleta manufaa kwa taifa ambayo ni kuongezeka kwa mapato yatokanayo na leseni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; ongezeko la walipaji wa kodi za mapato; Uendelevu wa shughuli za urasimishaji ambao unafanyika kwa gharama nafuu na kunaisaidia serikali kupunguza gharama za urasimishaji nchini. Aidha, kupungua kwa migogoro ya ardhi kumekuwa na faida kubwa kwa makundi mbalimbali yanayotumia ardhi ambayo sasa yanapata muda wa kufanya uzalishaji zaidi kuliko migogoro.

6.2.1. Ongezeko la Mapato yatokanayo na leseni za biashara



Vituo Jumuishi vya Urasimishaji na Uendelezaji biashara vimeongeza ukusanyaji wa mapato kwenye Halmashauri ambazo zimeshirikiana na MKURABITA kuanzisha Vituo hivyo. Vituo hivi vimewezesha upatikanaji wa huduma kwa haraka na bei nafuu. Jumla ya **Shilingi 385,755,000** zimekusanywa kutokana na ada za leseni katika Vituo vilivyoanzishwa kwa kipindi cha Mei 2020 hadi Juni 2020. Kati ya fedha hizo Shilingi **74,288,213** ni kwa ajili ya Halmashauri ya jiji la Mwanza, Shilingi **113,538,050** ni Halmashauri ya Mji wa Kahama, Shilingi **110,128,220** ni halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Shilingi **52,612,000** ni Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Shilingi **35,189,000** ni Halmashauri ya Mji wa Babati.

Vituo Jumuishi pia vimewezesha ongezeko la utoaji wa leseni za biashara kulinganisha na awali kabla ya uwepo wa Vituo. Katika Halmashauri ya Mji wa Njombe Kituo Jumuishi kimeongeza kasi ya utoaji leseni kutoka **2,125** kwa mwaka 2018/19 hadi kufikia **2,582** kwa mwaka 2019/20;

Mapato yatokanayo na leseni za biashara yameongezeka kutoka Shilingi **158,000,000** kwa mwaka 2018/19 hadi Shilingi **207,000,000** kwa mwaka 2019/2020.



Katika hatua nyingine, kuna ongezeko la idadi ya wamiliki wa biashara wa Halmashauri ya Mji wa Njombe wanaolipa kodi ya mapato, kutoka **asilimia 29** kwa mwaka 2018/2019 hadi **asilimia 70** kwa mwaka 2019/2020.



6.2.2. Uendelevu wa shughuli za urasimishaji

Baada ya kujengewa uwezo na MKURABITA, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imemiliki ajenda ya urasimishaji kwa kuendelea kupima mashamba **1,880** na kuandaa, kusajili na kutoa Hati za Haki Milki za Kimila **1,631** sawa na asilimia **89** ya mashamba yaliyopimwa.

6.2.3. Kupungua kwa migogoro ya ardhi

Uwepo wa Mipango ya matumizi bora ya ardhi umepunguza migogoro kati ya wakulima na jamii ya wafugaji baada ya vijiji kutenga maeneo ya makazi, makaburi, shule, ofisi za vijiji, Taasisi, eneo la malisho na kilimo. Vijiji **nane (8)** kati ya **39,** vya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi (sawa na **asilimia 20.5)** na Vijiji **57** kati ya **114** vya Halmashauri ya Wilaya Mufindi sawa na **asilimia 50** vina mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na Kamati za Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji (VLUM).

SURA YA SABA

RASILIMALI WATU NA FEDHA

Katika kuhakikisha shughuli za urasimishaji zinatekelezwa kikamilifu, usimamizi wa rasilimali watu na fedha ni muhimu ili kuleta tija katika utekelezaji na kupata thamani ya fedha inayotumika. Menejimenti imeendelea kusimamia rasilimali watu na fedha ili kuwezesha urasimishaji kufanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia thamani.

7.1 Rasilimali watu

Muundo wa sasa wa MKURABITA una uhitaji wa watumishi **27** kati yao watumishi **17** ni wa Idara ya Utawala na Fedha na watumishi **10** ni Idara ya Urasimishaji. Hadi kufikia Juni 2020, MKURABITA ilikuwa na watumishi **23** ambapo watumishi **7** ni Idara ya urasimishaji na watumishi **16** ni Idara ya Utawala na Fedha. Idadi ya watumishi kwa sasa ina upungufu wa watumishi wanne (4) kutokana na baadhi ya watumishi kustaafu na kufariki. Utaratibu wa kujaza nafasi zilizowazi unaendelea.



7.2 Mafunzo kwa watumishi



Mafunzo ya muda mfupi na mrefu yalitolewa kwa watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi. Mafunzo ya muda mfupi yaliyohusu mabadiliko ya kitabia *(Behavioral change)* katika utekelezaji wa shughuli za urasimishaji yametolewa kwa Watumishi 23. Watumishi watano (5) wamehudhuria mafunzo ya kitaaluma kwa mujibu wa Sheria za usimamizi na usajili wa Mamlaka zinazosimamia taaluma hizo. watumishi wengine

watatu (3) wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamili na wawili (2) mafunzo ya Diploma.

7.3 Vyanzo vya Fedha na Utekelezaji wa Bajeti

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo chanzo kikuu cha fedha za utekelezaji wa shughuli za MKURABITA kupitia fungu Na. 30 la bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, MKURABITA iliidhinishiwa bajeti ya **shilingi 4,143,086,600** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji na uendeshaji wa ofisi. Hadi kufikia Juni 2020, MKURABITA ilipokea **shilingi 2,955,053,794** sawa na **asilimia 71** ya bajeti**.** Utekelezaji wa shughuli za MKURABITA kwa mwaka 2019/20 umetumia **Shilingi 2,748,874,639** sawa na **asilimia 93** ya fedha zilizopokewa **kama** ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 13**

Jedwali Na. 11: Bajeti, Fedha iliyopokelewa na Matumizi kwa mwaka 2019/2020

Shughuli	**Bajeti**	Fedha iliyopokelewa	**Matumizi**	**Asilimia** fedha iliyopokelewa na Bajeti	**Asilimia ya Matumizi** na Fedha iliyopokelewa
Urasimishaji Ardhi	1,500,000,000	195,341,007	195,341,007	13%	100%
Urasimishaji Biashara	317,660,000	329,660,000	310,060,000	104%	94%
Ujengaji Uwezo	101,025,200	101,025,200	101,025,200	100%	100%
Huduma Saidizi	465,438,708	494,064,895	494,064,895	106%	100%
Uendeshaji wa Ofisi na Mishahara	1,758,962,692	1,834,962,692	1,648,379,537	104%	90%
Wastani	**4,143,086,600**	**2,955,053,794**	**2,748,870,639**	**71%**	93%

7.5 Ukaguzi wa Fedha za Utekelezaji

Ukaguzi wa shughuli za MKURABITA hufanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama ilivyo katika miaka yote ya utekelzaji wa MKURABITA katika ukaguzi wa Hesabu za mwaka 2019/20 MKURABITA pia ilipata **HATI SAFI**. Kiambatisho Na. 01 ni hesabu zilizokaguliwa za mwaka **2019/2020**.

KIAMBATISHO Na. 1: REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL STATEMENTS FOR THE PROPERTY AND BUSINESS FORMALIZATION PROGRAM FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020